Soma hadithi ifuatayo kisha ujibu maswali yanayofuata.

Baba yangu ni askari. Yeye huenda mafunzo ya askari kwa miezi minne. Sipendi akienda kwenye mafunzo. Kila wakati akienda sisi hubaki na mama na dada yangu mdogo.Wakati wa kwenda shuleni mama ndiye hunipeleka pekee. Mara nyingi rafiki yangu huniuliza kwa nini baba yangu hanileti shuleni. Naomba serikali ihakikishe baba anaenda mafunzo siku chache. Natamani kukaa na baba yangu. Ili kila siku amsaidie mama kutupeleka shuleni.

Maswali

1. Baba yake hufanya kazi gani? ***(Mwanafunzi ajibu)***
2. Baba huenda mafunzo miezi mingapi? ***(Mwanafunzi ajibu)***
3. Nani huwapeleka shuleni? ***(Mwanafunzi ajibu)***
4. Serikali ifanye nini? ***(Mwanafunzi ajibu)***
5. Familia hii ina watu wangapi? ***(Mwanafunzi ajibu)***

Zoezi 2: KUSOMA KWA SAUTI.

Soma kifungu kifuatacho kwa sauti.

Mimi hupenda kucheza. Michezo husaidia sana kunyoosha viungo vya mwili. Michezo pia hupunguza uwezo wa kupata maradhi kama vile kisukari. Wakati wa mapumziko, mimi hupenda kucheza soka. Mchezo huu huhusisha timu mbili. Kila timu hujitahidi kufunga mabao mengi iwezekanavyo. Ni vizuri kushiriki michezo ili kuboresha afya zetu.

SEHEMU 2: KUSOMA UFAHAMU. (Alama 10)

Ufahamu 1.

Soma hadithi ifuatayo kisha ujibu maswali yanayofuata.

Miti ni mimea mirefu na mikubwa. Miti hutumika kwa njia nyingi. Miti husafisha hewa. Hewa tunayopumua hutoka kwa miti. Miti pia hurembesha nchi yetu. Hufanya nchi kukaa safi na ya kupendeza. Miti hutupa chakula. Tunapata matunda kama maembe, mananasi, mapera na maparachichi. Miti pia ni dawa. Babu yangu mara nyingi akiumwa na tumbo, huenda mwituni kutafuta dawa. Akirudi huwa amebeba matawi. Anayachemsha kisha anakunywa.

Maswali

1. Miti ni mimea _____
2. Hewa tunayopumua hutoka wapi? _____
3. Miti hufanya nchi kuwa _____
4. Miti hutupa matunda kama yapi?
   _____
5. Babu kabla ya kunywa matawi hufanya nini _____